

Mkombozi

Empower. Engage. Enable.

Taarifa ya mwaka 2008: **KWA UFUPI**

Mkombozi

P.O. Box 9601
Moshi, Tanzania
Moshi tel: +255 27 2754793
Arusha tel: +255 272544319
info@mkombozi.org
www.mkombozi.org

Yaliyomo

uk.3 Ujumbe kutoka Mwenyekiti wa bodi ya wathamini
uk.4 Ulinzi
uk.5 Uwezeshaji
uk.6 Ushirikishaji
uk.7 Elimu
uk.8 Kujifunza
uk.9 Uvumbuzi
uk.10 "Katika maneno yao..."
uk.11 Taarifa ya Fedha 2008

Edited & designed by Tanja Kisslinger
Photos by Anna Thor

© 2009 Mkombozi

Mkombozi is a registered Tanzania Charity Trust (No. ADP / P12097)

Friends of Mkombozi is a registered UK Charity (No. 1101318)

Mkombozi ni nini?

Mkombozi ni shirika linalofanya kazi kuwasaidia watoto na vijana kukuwa kiakili, kimwili na kiroho. Tunataka kujenga jamii ambayo kila mmoja anamjali mwingine. Tunasaidia watu kuwaelewa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wale wanaoishi mitaani. Ndoto ya Mkombozi ni kuwa na dunia ambapo watu wote wanawapa umuhimu watoto na vijana - dunia ambapo vijana wanapata elimu, wanaishi maisha mazuri na wanafanya kazi kuendeleza jamii zao.

Mkombozi inasaidia watoto na vijana wa aina gani?

Watoto na vijana wasio na makazi na wanalala mitaani.
Watoto wanaoamua kuishi au kufanya kazi mitaani.
Watoto wanaokwenda mjini kuombaomba au wanafanya kazi mchana na kurudi nyumbani usiku.
Watoto wanaochukuliwa kutoka nyumbani kwao na kuletwa mjini kutumiwa na watu wazima.
Watoto walio katika hali ngumu sana majumbani mwao.
Watoto na vijana wanaojishughulisha na biashara ya ngono ili kujikimu.

Nini maana ya " Taarifa ya mwaka 2008: KWA UFUPI" ?

Mkombozi huandika "taarifa ya mwaka" kuonyesha utekelezaji wa shughuli na mafanikio kila mwaka. Kijitabu hiki ni muhstasari wa taarifa kamili ya mwaka 2008; ni toleo fupi na rahisi kwa wale ambao wanapenda kuipitia kwa haraka taarifa kamili. Muhstasari huu hutusaidia sisi kutoa taarifa ya shughuli na mafanikio yetu kwa watu wengi zaidi. Tafadhali furahia muhstasari huu wa kazi za Mkombozi kwa mwaka wa 2008 na baadhi ya matukio muhimu yaliyojiri katika mwaka huo.

Ujumbe kutoka Mwenyekiti wa bodi ya wathamini

2008 ulikuwa mwaka wa mafanikio makubwa na mafunzo kwa Mkombozi. Mabadiliko na fursa viliongoza mafanikio na changamoto za mwaka huu. Mkombozi ilishinda tuzo toka STARS Foundation, na hii ilithibitisha kwamba juhudi zake katika maendeleo zinathaminiwa dunia nzima. Pia inatambuliwa na kuthaminiwa kwa imani zake kuu na upendo ya kwamba watoto na vijana wana uwezo wa kukua kiakili, kimwili na kiroho tena kwa kiwango cha juu sana.

Waanzilishi wa Mkombozi walijali maendeleo, mabadiliko na moyo wa kibinaadamu. Mkombozi ilijengwa katika misingi ya upendo, imani na kufanya kazi kwa bidii, na imechukua safari ndefu kuwatia moyo na kuwawezesha watoto na vijana wa Tanzania kufikia ndoto zao. Waanzilishi walijitahidi kuwafikishia ujumbe watu wengi iwezekanavyo kwamba watoto lazima wahusishwe katika kufanya maamuzi yanayoathiri maisha yao.

Tunakumbuka kwamba, tuzo ya STARS ilitangazwa wakati ambapo Kate McAlpine alikuwa anaondoka na kumwachia William Raj jukumu la Ukurugenzi utendaji. William ataendelea kuongoza maendeleo ya Mkombozi, kuongeza mshikamano wa karibu na jamii, serikali za mitaa na watoto. Ni mtu anayejituma ambaye analeta watu pamoja.

Kwa ujumla, mwaka 2008 ulikuwa mwaka wa mabadiliko na kukuwa, pia kujifunza na kuendelea. Mimi binafsi nafurahi kuwa sehemu ya mafanikio endelevu ya Mkombozi.

Kara Kirby

Ulinzi

Mkombozi inathamini ulinzi kwa mtoto na kijana kwa sababu kumlinda mtoto maana yake ni kumkinga na hatari mbalimbali. Watoto ni watu muhimu wenye haki ya kulindwa na watu wazima wanaowajali.

Kwa ufupi kuhusu ULINZI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2008...

- ⓘ Huduma za afya zilitolewa kwa vijana zaidi ya mara 2000.
- ⓘ Milo 76,230 ilitolewa kwa watoto na vijana wanoishi au kusoma Mkombozi.
- ⓘ Watoto wote kituoni walipimwa na kufuatiliwa urefu na uzito wao.
- ⓘ Wamama vijana 7 walifundishwa jinsi ya kutunza na kulisha watoto wao.
- ⓘ Zaidi ya vijana 50 walisaidiwa kupima VVU NA UKIMWI.

Mkombozi ilishinda tuzo ya STARS ya kazi bora kwa mwaka 2008! Mkombozi inafanyakazi kuhakikisha kwamba watoto wako salama. Kwa mfano, tunawasaidia watoto wanaoishi au kufanya kazi mitaani, tunaelimisha walimu kuhakikisha usalama wa watoto wawapo shuleni, tunatafuta msaada wa kisheria kwa ajili ya watoto walionyanyaswa na tunashirikiana na jamii kuwalinda watoto majumbani na katika mazingira yanayozunguka nyumbani. Mwaka 2008 Mkombozi ilishinda tuzo kubwa kwa kufanya kazi hii. Tuzo hii ilitolewa na STARS Foundation, shirika lenye makazi yake huko Uingereza.

"Tulinde watoto sasa!" - Kuelimisha jamii kuhusu unyanyasaji wa watoto: Watoto wengi wanaoishi mitaani wameondoka majumbani mwao kwa sababu walinyanyaswa. Mkombozi inadhani kwamba unyanyasaji wa watoto ni kosa na kwamba haupaswi kutokea kwa sababu unaumiza watoto kimwili, kihisia na kiroho. Tunaamini inaweza kuzuiwa kama watu watajifunza ni kwa kiasi gani unyanyasaji unaumiza watoto. Mwaka 2008, Mkombozi ilianza kampeni ya 'Tulinde watoto sasa!'. Kampeni ilielimisha jamii kuhusu unyanyasaji kupitia maigizo ambayo yalionwa na watu wapatao 2000 katika miji ya Arusha na Moshi. Pia Mkombozi ilimsaidia mtoto ayekuwa amenyanyaswa kutoa taarifa kituo cha polisi na kesi kufikishwa mahakamani.



Mkombozi inathamini uwezeshaji wa vijana kwa sababu vijana wenye elimu na kazi wanaweza kupata pesa kujilipia gharama zao na familia zao; hawahitaji msaada wa mkombozi tena.

Kwa ufupi kuhusu UWEZESHAJI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2008...

- Wavulana 8 na wasichana 5 walifunzwa jinsi ya kuendesha biashara zao wenyewe.
- Wavulana 11 na wasichana 8 walisaidiwa kupata ajira sehemu mbalimbali.
- Vijana 28 walifundishwa jinsi ya kufanya maombi ya kazi na tabia njema kazini.
- Vijana 7 walifundishwa jinsi ya kutengeneza karatasi.
- Vijana 10 wanaoishi katika kituo cha Mkombozi walisafiri Uingereza kucheza rugby.

Wasichana sita walipata kazi baada ya kozi ya hoteli menejimenti! Mwaka 2008, Mkombozi iliwasaidia wasichana sita waliokuwa wakiishi katika mazingira magumu, kufanya kozi ya hoteli menejimenti, na walifundishwa jinsi ya kuomba kazi. Walipomaliza kozi kila mmoja alipata ajira katika hoteli /mgahawa tofauti. Sasa wanaweza kujilipia kodi ya nyumba na chakula.

Wavulana walikuwa wanasarakasi na wakaacha maisha ya mitaani: Mwaka 2008, Mkombozi iliwakaribisha vijana wanaoishi katika mitaa ya Arusha kuwa wanasarakasi. Baada ya mafunzo ya muda mrefu, baadhi ya vijana hawa waliamua kurudi na kuishi na familia zao na kwenda shule. Haya yalikuwa mafanikio makubwa. Vijana walioendelea na mafunzo ya sarakasi waliacha kuishi mitaani na sasa wanakodisha vyumba vyao wenyewe.

Wavulana wanne walirudi vijijini kwao baada ya kujifunza kuendesha biashara: Mkombozi inafundisha vijana jinsi ya kuendesha bishara ndogondogo; Kwa mfano kuuza mchicha sokoni. Mwaka 2008 wavulana wanne walirudishwa kwenye familia zao katika vijiji mbalimbali baada ya kujifunza kuendesha biashara. Familia zao ziliwakaribisha na walifurahi kwamba waliweza kutengeneza kipato.

Mwanamke kijana amewezeshwa kwa kujifunza jinsi ya kuendesha biashara ndogondogo.

Ushirikishaji

Mkombozi inathamini ushirikishaji wa jamii kwa sababu watu, jamii na serikali lazima wahakikishe kwamba watoto wote ni salama, wanafuraha na wanajaliwa.

Kwa ufupi kuhusu USHIRIKISHAJI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2008...

- Walimu 45 kutoka shule 9 walifunzwa kufundisha watoto kuwa waulizaji wa maswali wanaofikiri.
- Viongozi 100 wa serikali za mitaa walifunzwa kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.
- Mamia ya wanajamii walikuja Mkombozi kuangalia maonyesho ya maigizo ya vijana ya kila mwezi.
- Vijana wa Mkombozi walishiriki mashindano mbalimbali yakiwemo yale ya Kilimanjaro Marathoni.

Kaka Mkubwa na Dada Mkubwa: Wapo watoto wengi ambao hawana mtu mzima wa kuwajali. Watoto wote wanataka mtu mzima kuwa karibu nao, kuongea nao, kutumia muda nao ili wasijisikie wapweke. Katika Mkombozi, watu hujitolea kuwa "Kaka Mkubwa" au "Dada Mkubwa" na kuwasaidia watoto kwa kuwa rafiki yao. Kwa mwaka 2008 watoto kumi na nane walipata Kaka au Dada Mkubwa.

Kufanya kazi kwa ushirika na serikali huko Arusha: Mkombozi inafikiri ni muhimu kushirikiana na serikali. Oktoba 2008, Mkombozi iliwakaribisha wafanyakazi wa serikali katika mkutano wa jinsi ya kuwalinda watoto uliofanyika Arusha. Washiriki walijumuisha wawakilishi kutoka maendeleo ya jamii na idara ya ustawi wa jamii, polisi na Mkuu wa wilaya - Mheshimiwa Evance Balama.

Wanajamii wa Moshi waliweka matarajio ya baadaye: Mkombozi inafanya kazi na jamii (viongozi wa kijamii, walimu na wazazi) kuwasaidia watoto katika nyumba zenye matatizo. Wanajamii wa Moshi walitupatia mawazo ya thamani kwa ushirikiano. Kwa mfano, wangependa familia zielimishwe kuhusu malezi ya watoto na wangependa viongozi wa kijamii kuweza kuwatambua watoto wenye matatizo.

Kaka Mkubwa wa Mkombozi na kijana wakipanda mti katika shule ya jamii.

Mkombozi inathamini uwezeshaji wa vijana kupitia elimu kwa sababu inawapa vijana katika mazingira magumu nafasi kwa maisha bora. Inafanya hilo kwa kuwapatia ujuzi, maarifa na fursa mbalimbali.

Kwa ufupi kuhusu ELIMU ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2008...

- ⓘ Wahitimu 6 wa MEMKWA na watoto 81 walisoma primari na sekondari.
- ⓘ Watoto 9 walifanya mitihani ya taifa na walihitimu darasa la saba.
- ⓘ Watoto wote waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2007 walijiunga na sekondari.
- ⓘ Darasa la komputa lenye komputa 16 lilifunguliwa kwa ajili ya watoto katika kituo cha Mkombozi.

Vijana 1589 walifunzwa jinsi ya kutumia komputa! Mradi wa komputa wa Mkombozi unaojihusisha na komputa za bei nafuu (ACTT) unauza komputa zilizotumika na unafunza vijana jinsi ya kutumia komputa. Mradi huu pia unasaidia mashule kufungua madarassa ya komputa - Madarasa 18 yalifunguliwa mwaka 2008. Katika madarasa yote ya komputa yaliyoanzishwa na ACTT vijana 1598 wamefundishwa kutumia seti ya komputa.

Mobile Unit - Basi lenye darasa ambalo linazunguka katika mitaa ya mji wa Moshi: Mwaka 2008 Mkombozi ilipatiwa coaster ambalo linatumika kama darasa linalotembea. Katika coaster hii, watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani wanaweza kujifunza kusoma, kuandika, kuhesabu, afya na haki za watoto. Madarasa yanayotembea huwasaidia vijana hawa kujisikia vyema kuhusu wenyewe na kugundua vipaji vyao.

Kwenda shule kulibadilisha maisha ya watoto: Mwaka 2008, vijana wote wanaoishi Mkombozi ambao walikuwa tayari kwenda shule walifanya vizuri katika masomo yao. Hata vijana wenye umri wa miaka kumi walihamia shule za bweni. Kusoma kunabadilisha maisha yao; wanajisikia vyema juu ya yale wanayofanya na pia wanapata nafasi kutumia muda wao na watoto wengi wengine na vijana. Mkombozi inafuraha kuona watoto hawa wanachukua wajibu kama huu kwa masomo yao.



Wanafunzi katika darasa la komputa Mnini lilianzishwa kwa ushirikiano na ACTT.

ⓘ Kujifunza

Mkombozi inathamini kujifunza maisha mazima kwa sababu kupitia kujifunza kwa kila siku ndipo tunapogundua mambo mapya ambayo kwa hayo tutaboreka zaidi na zaidi katika kufanya kazi na watoto na vijana.

Kwa ufupi kuhusu KUJIFUNZA ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2008...

- ⓘ Vijana 22 waliweza kuishi pamoja katika nyumba za vikundi vidogo vidogo baada ya kuondoka kituoni.
- ⓘ Watoto 18 waliishi na wazazi walezi (watu wazima ambao sio ndugu zao) kwa vipindi vifupi.
- ⓘ Watoto wanaoishi kituoni waliendesha mikutano ya watoto mara moja kila baada ya wiki mbili.
- ⓘ Vijana wanaolala mitaani walipewa sabuni, dawa ya mswaki na mafuta ya kujipaka.
- ⓘ Wavulana 9 na Wasichana 14 walijiunga na mafunzo ya siku tano ya VVU na UKIMWI yaliyoendeshwa katika shule ya sekondari ya Arusha Meru.

Ni vyema watoto kuishi na familia zao kuliko kituoni: Tangu Mkombozi ilipoanzishwa, watoto wengi wameishi katika kituo chetu kilichopo katika mji wa Moshi. Baadhi wamekaa kwa muda mfupi wengine kwa miaka mingi. Mkombozi imejifunza kwamba si vizuri kwa watoto kuishi katika kituo kwa muda mrefu kama huo - Wanajisikia furaha kuishi katika familia inayowajali. Mkombozi sasa inajua kwamba watoto wanapaswa kuishi kwa muda mfupi tu kituoni. Wanapokuwa pale tutatafuta wapi ni mahali bora kwa wao kuishi. Watoto wengine wanaweza kurudi na kuishi na famila zao, au wanaweza kuishi na ndugu au mtu mzima ambaye hata sio ndugu. Kama wana umri wa kutosha wanaweza kuishi wenyewe au hata na marafiki. Watoto wanakimbia nyumbani kutokana na matatizo katika familia, na mara nyingi matatizo haya yanaweza kutatuliwa. Mkombozi itaanza kufanya kazi zaidi ya kuzisaidia familia kutatua matatizo yao ili watoto waweze kurudi nyumbani badala ya kuishi kituoni kwa muda mrefu. Bado, kituo ni muhimu kwa muda mfupi kwa sababu ni hatari sana kwa mtoto kuishi mitaani.

Baadhi ya vijana (wanaoishi katika kituo cha Mkombozi) wakiwa kwenye safari.

Mkombozi inathamini uvumbuzi kwa sababu tunawasaidia watoto na vijana kupata maisha bora, na tunawaelimisha watu kuhusu haki za watoto. Kazi hii siku zote inahitaji mawazo mengi mapya.

Kwa ufupi kuhusu UVUMBUZI ndani ya Mkombozi kwa mwaka 2008...

- Watoto 24 na vijana walirudishwa nyumbani kuishi na familia zao.
- Mkombozi ilidhamini siku ya michezo kwa watoto wote wanaoishi/ kufanya kazi katika mitaa ya mji wa Moshi.
- Mradi wa ACTT wa Mkombozi ulifungua biashara ya intaneti mjini Moshi.
- Watoto wanaolala mitaani walitembelewa na mfanyakazi usiku mara moja kwa wiki.
- Safari kadhaa zilifanywa kuwatembelea vijana walioko mahabusu.

Mkombozi imepata Mkurugenzi mpya! Kwa miaka 11 Mkurugenzi wa Mkombozi alikuwa Kate McAlpine. Mwaka 2008, aliacha Mkombozi na kukabidhi jukumu la ukurugenzi kwa William Raj. Hivi ndivyo asemavyo William kuhusu yeye kuwa kiongozi mpya wa Mkombozi: “Nathamini kazi za Mkombozi zinamrudishia mtoto thamani ya kuwapo kwake na matumaini ya maisha. Ndoto yangu kama kiongozi ni kuwa mtu anayejali na mwenye kanuni anayeamini kwamba mwanadamu anawezafanya chochote. Nataka kuwatia moyo wafanyakazi, watoto na wengine tunaofanya nao kazi kushiriki katika ndoto hii - na kuelewa kwamba wanaweza kujiendeleza wenyewe na Tanzania. Mitaa haizai watoto - ni sisi na watoto ni wa kwetu. Basi tushughulikie maswala ya watoto na vijana kwa mtazamo wa kiufumbuzi na sio kama matatizo yaliyoshindikana.”

Watoto wasiitwe “watoto wa mitaani”: Watoto wanaishi mitaani kwa sababu kuna matatizo mengi manyumbani mwao na hawapendi kubaki hapo. Wanapoondoka majumbani kwao, hakuna mtu wa kuwasaidia. Mwaka 2008, Mkombozi iliamua kuacha kuwaita hawa "watoto wa mitaani", kwa sababu watoto wote wanatoka katika familia na sio mitaani. Mitaa haiwezi kulea mtoto, ni watu wazima tu wanaowajali ndo wanaweza.

Watoto katika shule inayotembea (Mobile School) katika kipindi Arusha.

Katika maneno yao...

"Sasa hivi wamenitafutia kazi na nipo nafanya kazi. Na baada ya miezi 3 nitatafuta maisha yangu peke yangu huku nikiendelea kufanya kazi. Katika miezi 6 nimepata naona mabadiliko sababu nilikuwa nikiwaza sana nitaishije. Ambapo sasa nimejua nitakavyoishi maana nimepata kazi. Na hata kama maisha yakiwa magumu sana ninajua jinsi ya kutumia budget. Kwani nilivyokuwa nikikaa group housing nilifundishwa jinsi ya kutumia budget. Badiliko hili ni la msingi kwa sababu limenitengeneza kimaisha. Kwani bila badiliko hili ningeishi katika maisha magumu sana. "

Mama kijana anaeleza jinsi Mkombozi ilivyomsaidia kupata elimu na kazi.

"Mkombozi imenisaidia silali tena mtaani, sikosi chakula na nimebadilisha maisha yangu ya kukaa mtaani kwani sasa nina kitu cha kufanya mimi sio tena mtoto wa mitaani."

Kijana mvulana anaelezea jinsi Mkombozi imebadilisha maisha yake.

"Kilichonifurahisha ni kuja kusoma MEMKWA kukaa na wenzangu kwa amani na usalama wangu. Kwani nilipokuwa mtaani nilikuwa na hofu ya maisha yangu. Nilikuwa natishwa sana na watu kutokana na hali yangu (zeru zeru). Kwa sasa Mkombozi nafaidi elimu na usalama wa maisha yangu. Najua kusoma na kuandika. Badiliko hili ni la msingi kwa sababu nataka elimu."

Mtoto wa Mkombozi anaelezea jinsi maisha yake yalivyobadilika tangu alipojiunga na Mkombozi.

Maelezo ya taarifa za fedha

kwa mwaka uliomalizika 31 Disemba 2008

(Taarifa hizi zimeandaliwa katika shilingi za kitanzania)

MAPATO

RUZUKU	
Terre Des Hommes	21,315,510
Comic Relief	303,355,006
Foundation for Civil Society	108,779,262
Friends of Mkombozi	103,356,433
Railway Children	73,336,944
International Child Support	158,150,000
Street Kids International	19,276,000
Church World Service (CWS)	9,252,968
Pilgrim Foundation	3,498,202
Research on Poverty Alleviation	9,377,550
Pestalozzi	113,754,428
Donations	20,511,162
JUMLA YA MAPATO	943,963,465

MATUMIZI

PROGRAMMES	1,003,972,709
ACTT	31,605,024
Other	19,691,442
JUMLA YA MATUMIZI	1,055,269,175

Mkombozi

P.O. Box 9601
Moshi, Tanzania
Moshi tel: +255 27 2754793
Arusha tel: +255 272544319
info@mkombozi.org
www.mkombozi.org